

AAAP N° 37

SWAHILI FORUM I



MÄRZ 1994

Edited by
Rose-Marie Beck
Thomas Geider
Werner Graebner

Afrikanistische Arbeitspapiere
Institut für Afrikanistik
Universität zu Köln
50923 Köln
Germany

© by the editors

ISSN 0178-725X

**Kiinimacho cha mahali:
kiambishi tamati cha mahali -ni**

Ridder Samsom na Thilo C. Schadeberg
Chuo Kikuu cha Leiden

The locative suffix *-ni*

In this article we discuss two hypotheses about the origin of the locative suffix *-ni*. The better known hypothesis (Raum 1909; Meinhof 1941/42) assumes that the suffix *-(i)ni* developed out of a class 18 demonstrative, though the details of the assumed phonological changes have never been made clear. The competing hypothesis by Sacleux (1939) suggests that locative nouns with *-ni* started out as compounds with the noun *ini* 'liver'. We think that this second hypothesis is phonologically more plausible and that it also accounts for the specific link with the meaning of class 18 'inside'. Comparison of the spread of the locative suffix *-(i)ni* and of the word *ini* 'liver', together with other historical considerations, point to Kiswahili (or Sabaki) as the most likely origin of this locative suffix.

1. Utangulizi

Makala yetu inahusu asili na usambazaji wa kiambishi tamati cha mahali *-ni*. Katika lugha karibu zote za Kibantu kuna ngeli tatu za mahali zenye viambishi hivi vitatu: *pa*, *ku* na *mu*. Katika lugha ya Kiswahili mofimu hizi zinatumiwa sana kama viwakilishi, kwa mfano katika viwakilishi vionyeshi *hapa*, *huku*, *humu*, tena katika viwakilishi vimilikishi, kwa mfano *kwao*. Tunavikuta pia kama viambishi vya vitenzi, kwa mfano *hapapitiki*, *kumekucha*, *hamna*. Matumizi yake kama viambishi vya kijina yako katika vivumishi tu, kwa mfano *pazuri*. Lakini majina yenyewe, kwa kawaida, hayatokei pamoja na viambishi awali vya ngeli hizi, isipokuwa maneno machache ambayo bila shaka yameundwa hivi hivi zamani, kwa mfano *kuuke* na *kuume*, *kushoto*, *kuzimu* na machache mengineyo.

Bali, tunapotaka kutaja mahali pa kitu fulani, kwa mfano ‘kwenye nyumba’, hatuwezi kuongeza kiambishi awali cha mahali, lakini inatubidi kuongeza kiambishi tamati *-ni*, kwa mfano *nyumbani*. Jina pamoja na kiambishi tamati *-ni* likawa ni jina la ngeli ya 16 (*nyumbani pale*), au ya 17 (*nyumbani kwetu*), au ya 18 (*nyumbani humu*).

Tunajua kwamba, hii si hali ya Kibantu cha asili kwa sababu lugha nyingine, kwa kawaida, hutumika viambishi awali hivi pamoja na majina, kwa mfano, Wagogo wangesema *ha-nyumba, ku-nyumba, mu-nyumba*. Lugha zenye kiambishi tamati *-ni* ni chache, na zote ziko Afrika Mashariki na Afrika Kusini, na hasa haziko mbali na mwambao wa Bahari ya Hindi. Lugha hizo zinaonyeshwa kwenye Ramani 1.


Orodha hii inafuata tasnifu ya Claire Grégoire (1975, uk. 185-204) inayohusu ngeli za mahali katika lugha za Kibantu. (Tumeiondoa lugha ya Kinyamwezi ambayo haitumii kiambishi tamati *-ni* isipokuwa katika maneno machache yaliyoazimiwa kutoka lugha ya Kiswahili. Tena tumeongeza lugha ya Kirangi.)

Katika baadhi ya lugha hizo kiambishi si *-ni* lakini *-ini*. Irabu *i* ya mwanzoni inasikika vivyo hivyo katika Kikikuyu, kwa mfano *nyumba-ini*, na pengine katika Kizulu, kwa mfano *ezulwini* ‘mbinguni’ < *iizulu*; katika lugha nyingine (kwa mfano E.60, S.30, S.40) hujiunga na irabu itanguliayo; kwa mfano Kisotho ya Kaskazini (S.32) *tsele* ‘njiani’ < *tsela*; Kichaga (E.62) *mringeny* ‘majini’ < *mringa*. Kwa hiyo inakubalika kwamba mofimu hii mwanzoni ilikuwa ina umbo la *-ini*.

Basi, swali ambalo tungependa kulijibu ni: Mofimu hii limetungwa vipi, na wapi, na lini.

2. Dhanio la Raum-Meinhof

Carl Meinhof, katika makala iliyotolewa 1942, alipendekeza kwamba asili ya kiambishi tamati *-ni* ni kiwakilishi kionyeshi cha ngeli ya 18 yenye umbo la *imwi*. Anavyoona Meinhof, kiambishi awali *mu-* ikalainika, ikawa *m-* na baadaye ikatoweka kabisa. Kwa hiyo, watu wakaanza kuongeza kiwakilishi kionyeshi chenye maana ya ‘humu’ au ‘humo’. Meinhof anadai pia kwamba umbo la *mu* inaweza kugeuka *ni*: badiliko lilo hilo limetokea katika mofimu ya nafsi ya pili (wingi) ambayo ni *mu* kama kiambishi cha kitenzi lakini inaonekana kama *nyi* au



- | | | | |
|------|--------------------------------|------|---------------------------|
| E.50 | Kikikuyu, Kikamba ... | S.20 | Kivenda |
| E.60 | Kichaga (Machame ...) | S.30 | Kisotho, Kitswana |
| E.70 | Kipokomo, Kitaita ... | S.40 | Kinguni (Kizulu, Kixhosa) |
| F.33 | Kirangi | S.50 | Kitsonga |
| G.20 | Kipare, Kisambaa, Kibondei ... | S.60 | Kitonga cha Inhambane |
| G.36 | Kikami (si lazima) | | |
| G.40 | Kiswahili | | |
| G.62 | Kihehe (si lazima) | | |
| P.30 | Kimakua, Kilomwe | | |

ni ikitumiwa kama kiwakilishi nafsi huru, yaani *ninyi*. Kwa kweli, dhanio hilo limeshapendekezwa katika sarufi ya Kichaga iliyotolewa 1909. Mwandikaji Raum anasema (uk. 58): “Die Ortssilbe *mu* hat sich im Motschi nur als Suffix am Nomen erhalten als Lokativsilbe *ni*. Der Wechsel im Nasal ist in der unbetonten Endsilbe begreiflich; er hatte zur weiteren Folge den Umlaut von *u* in *i*.”

Grégoire anaona hoja nne zinazoweza kuimarisha dhanio la Raum–Meinhof:

- Kwanza, si kitu cha kigeni kutumia kiwakilishi kionyeshi cha mahali pamoja na jina ili kuimarisha maana ya mahali. Hii inatokea katika baadhi ya lugha za Kibantu za Afrika Mashariki.
- Ya pili, eneo la *-ini* na eneo ambalo kiambishi awali *mu-* hulainika yanafanana.
- Ya tatu, katika lugha ya Kigusii (E.42) kuna kihusishi *imi* yenye maana ya ‘katika’ inayofuata jina. Grégoire anafikiri kwamba labda neno hilo (au neno kama hilo) ni asili ya kiambishi tamati *-ni*.
- Ya nne, inaonekana kwamba kiambishi tamati *-ni* kina uhusiano maalum na ngeli ya 18 yenye maana ya undani. Uhusiano huu unaonekana katika neno la zamani sana *ndani* ambalo ni la ngeli 18 (neno *nda* yenye maana ya ‘tumbo’ limetoweka katika lugha ya Kiswahili); lakini hapana neno kama hili kutokana na ngeli ya 16 au 17. Tena, katika lugha ya Kitonga cha Inhambane (S.62, Msumbiji) vipo viwakilishi vionyeshi vya ngeli za 16 na 18, lakini kile cha ngeli ya 16 hakiwezi kutumika pamoja na jina lenye kiambishi cha mahali *-ni*.

Hoja tatu za kwanza hazina nguvu sana. Hoja ya kwanza inaonyesha kwamba muundo huo unawezekana, lakini haionyeshi zaidi. Hoja ya pili ina tatizo fulani. Kuna baadhi ya lugha ambazo hutumia *-ni* badala ya kiambishi awali cha mahali *mu-*, lakini viambishi vyenye umbo lilo hilo vya ngeli za 1 na za 3 bado vipo katika lugha hizo bila kulainika. Hoja ya tatu, pia, haitusaidii sana: ingawa asili ya neno hilo *imi* haijulikani hakuna sababu yoyote kufikiri kwamba inatokana na kiwakilishi kionyeshi cha ngeli ya 18. Inayobaki ni hoja ya ya mwisho, yaani maana ya *-ni* si mahali popote lakini hasa undani.

Upande mwingine kuna sababu ya kupinga dhanio la Raum–Meinhof. Inatubidi kuisitiza kwamba kiwakilishi cha mahali cha Kiherero *imwi* ‘humu’, ambacho Meinhof alifikiri kwamba ni asili ya *-(i)ni*, hakijulikani katika maenezi la kiambishi tamati cha mahali *-ni*; tena kanuni za kubadilisha *imwi* ikawe *ini* si wazi kabisa.

3. Dhanio la Sacleux

Charles Sacleux ametoa maoni tofauti juu ya asili ya kiambishi tamati *-ni*. Katika Kamusi yake maarufu (1939) anasema kuwa kiambishi tamati hicho kinatokana na neno *ini* ambalo tafsiri yake kwa Kifaransa ni 'foie, partie intime'. Haelezi zaidi ila katika lahaja moja ya Kiteita, yaani Kidavida, watu husema *nyumbêni* kufuatana na msinyao wa *nyumba* na *ini: nyumba-ini*. Sacleux hakutoa sababu nyengine au maelezo zaidi nao wataalamu wengine wa lugha za Kibantu hawajapata kuangalia fikra hiyo.

Basi nasi tujaribu kukadiria uwezekano wa fikra hiyo kuwa kiambishi tamati *-ini* inatokana na jina *ini* lenye maana ya 'kinofu chekundu cha ndani ya mwili kilichojaa damu na kinachotoa nyongo kusaidia kuyeyusha chakula tumboni' (A. S. Nabhany, *Kando ya Kiswahili*, muswada).

Maenezi ya shina *ini*:

Ramani 2 inaonyesha lugha zilizo na neno *ini* lenye maana tuliyotaja hapo juu. Katika lugha nyengine tunayakuta mashina mbalimbali kwa maana ya 'ini' kama vile: *-tima*, ambalo lina maana ya 'moyo' kwa lugha nyengine. Mashina mengine tupatayo ni *-toga*, hasa katika lugha za eneo la P, na *-bindi* katika lugha za eneo la S.

Basi tukitazama maenezi haya, tunaona maenezi hayo hasa ni katika lugha za Kisabaki, na lugha chache nyengine huko na huko katika Kenya, Tanzania na Uganda. Mojawapo ya lugha hizi iwe asili ya kiambishi tamati *-ini*.

Maana ya neno *ini*:

Tukichambua maana na matumizi ya neno *ini* kwa Kiswahili, tunaona mambo mawili: (1) Neno la *ini* au zaidi *maini* hutumika tu kwa maana ya 'kiungo cha ndani'. (2) Mnyambuliko wa jina *ini* katika ngeli ya 7, yaani *kiini*, unatumika kwa maana yafuatayo: Sacleux (1939) anaeleza kuwa maana yake hasa ni *coeur d'une chose*, 'moyo wa kitu', ambayo ni hasa sehemu ya ndani iliyo muhimu kuliko zote. Kwa mfano *kiini cha karafuu* ni kama 'chembe' au 'punje' ya karafuu. Neno la *kiini* pia hutumika kwa njia ya sitiari, naye Sacleux anatoa mfano huo: *Pate ndiyo kiini cha ungwana*, yaani kisiwa cha Pate kiwe chanzo au asili ya ustaarabu. Mifano mingine ni *kiini cha jicho* kwa 'mboni' (Sacleux

anatoa *kiini cheusi* na *kiini cheupe*), *kiini cha yai*, na hilo neno pacha tulilotumia katika jina la makala yetu *kiini macho* (ingawa hapo Krapf 1882 anatoa asili tafauti kabisa: *kilimato* < *killamato!*).

Sacleux anatofautisha kati ya *kiini cha mti* na *moyo wa mti*, kwa maana ya kuwa *kiini cha mti* ni undani wa mti ulio mgumu sana, nao *moyo wa mti* ndani yake iwe laini.

Kwa jumla tunaweza kukubali kuwa maana ya ‘undani’ au ‘ndani ya’ yangefaa kama asili ya kiambishi cha mahali *-ini*. Maana hayo zaidi yangeambatana na ngeli ya *mu-*, ngeli ya 18. Mifano michache ya Kiswahili cha zamani inaonyesha muungano huu wa kiambishi tamati cha mahali *-ni* na ngeli ya 18. Katika tasnifu yake (1979) Bi Mieke anataja mifano hiyo ya kiunganishi cha ngeli 18 kilichounganishwa na majina yaliyo na kiambishi tamati *-ni*: *ndani* na *chini* (*tini* kwa Kimvita).

Katika Utendi wa “Das Geheimnis der Geheimnisse” (Dammann 1940:222, ubeti 71) kuna sehemu hii:

<i>na ndani mwa kitambaa</i>	Und drinnen in dem Tuch
<i>tja hoyo mbwa juhaa</i>	jenes unwissenden Hundes,
<i>asozuru, asofaa</i>	der weder Schaden noch Nutzen aufweist,
<i>mtokozwa ni azizi</i>	der von den Mächtigen verstoßen wird,

Mfano mwengine unatokana na “Utendi wa Fatuma” (Dammann 1940:116, ubeti 213):

<i>na wakuteneo kwake</i>	Auch zu denen, welche sich versammelt haben
<i>tini mwa arishi yake</i>	unter seinem oberen Thron,
<i>shani lao liwafike</i>	ist ihre Herrlichkeit gekommen,
<i>wothe pia kwa ajaa</i>	zu ihnen allen in Eile.

Kiswahili cha siku hizi pia kinaonyesha uwezekano wa kuunganishwa kwa njia hiyo, kwa mfano: *miongoni mwa ...*, *kusini* (au *kaskazini*) *mwa ...*

Maana hayo ya ‘kiungo cha ndani’ kuwa asili ya maana ya ‘ndani ya’ au ‘undani’ na mwishowe kwa mahali, si ajabu. Walivyoeleza Heine, Claudi na Hünнемeyer (1991) mara nyingi viungo vya mwili hutokea kama dhana za mahali, ingawa kwa maana ya ‘katika’ hasa maneno kama ‘tumbo’ hutumiwa, kama vile hilo neno la Kiswahili *ndani* < **nda-ni*. Hata hivyo, neno lenye maana


ya '(ma)ini' limepata maana ya 'ndani (ya)' katika lugha ya Kingbandi (Afrika ya Kati); mabadiliko hayo hayo ya maana yametokea katika baadhi ya lugha za visiwa vya Pasifiki (Heine et al. 1993:140).*

Kwa kweli tumetafuta sana kupata matumizi mengine ya neno la Kiswahili *ini* au *maini* ambayo yawe tamathali, yaani si maana halisi tu. Hatukupata, ila msemu *maneno ya kukata ini* (Ndalau na King'ei 1988:65) au *maneno yake yalinikata maini* (Sauda Barwany, mawasiliano ya kibiniafsi) tu. Maana yake ni kufuatana na Ndalau na King'ei 1988: "maneno ya kumkera na kumuudhi mtu"; kufuatana na S. Barwany maana ni 'maneno yanamwumiza huyo mtu'. Tena katika methali au misemo mingine hatukupata. Scheven 1981 naye pia hana kiungo cha *maini* katika orodha yake. Ukiuliza "Hii ndiyo nini?", mtu anaweza akakujibu "Maini, moja lako moja la Salimini". Basi, hatuna misemo zaidi. Pengine hii inathibitisha kuwa kwa Kiswahili maana yenye sitiari au maana tamathali zaidi yanatolewa na maneno kama *moyo* au *mtima* nalo hilo neno *(ma)ini* limepata hasa maana ya kiungo halisi na baadaye maana ya mahali.

Kuunganisha kwa maneno:

Ikiwa tunakubaliana na fikra ya Sacleux kuhusu asili ya hiyo *-ini* ya mahali, inatulazimu tuthibitisha uwezekano wa kuunganisha kwa maneno mawili yawe neno pacha: neno la kwanza liwe jina lolote, neno la pili ni *ini*. Kwa kweli kwa Kiswahili si rahisi kuunganisha majina mawili ilivyo katika lugha nyingine. Yako maneno ambayo yameundwa kutokana na maneno mawili kwa kupoteza kiunganishi *-a* katikati, kama vile *gari (la) moshi, maji (ya) moto, msu (wa) meno*. Hapo jina la pili hueleza kitu kuhusu jina la kwanza: msumeno si meno ya msu, lakini ni msu wenye meno; majimoto si moto wa maji, bali ni maji yenye moto; garimoshi si moshi la gari, lakini ni gari lenye moshi. Kufuatana na msingi huu tunaweza tukasema *nyumba ini* si ini la nyumba, yaani ndani ya nyumba, lakini nyumba yenye ini.

Mfano kama huu wa kuwa kiangama ni jina linalotokea baada ya jina la kwanza, tunakuta pia katika lugha ya Kiilwana: *nyuuba mibeeni*, yaani 'katika nyumba' (tafsiri halisi: nyumba mimbani; D. Nurse, mawasiliano ya binafsi).



- Lugha zote za Sabaki, yaani lahaja mbalimbali ya Kiswahili, lahaja za Mijikenda, lahaja za Kipokomo, lahaja za Kikomoro — isipokuwa lugha ya Kiilwana
- Kikiyuyu (E.51) *iini* (lugha nyingine za kundi la Kenya ya Kati zinatumia neno *mtima*)
- Kinyankore (E.13) *ekine*
- Kihaya (E.22) *ine*
- Lumasaba (E.31) *khiini*
- Kilugulu (G.35) *kini*
- Kisambaa (G.23). Kizaramo (G.33) *ini*

4. Chanzo na usambazaji

Tukubali kwanza kwamba kiambishi tamati *-ini* katika lugha zote zionyeshwazo kwenye Ramani 1 kina asili moja. Ni wazi kwamba lugha hizo si tawi moja la lugha za Kibantu; kwa hiyo tukubali tena kwamba kiambishi hicho kimesambaa kutoka lugha moja. Kuna lugha moja tu ambayo imeenea kadiri ya kutosha ya kuwa chombo cha kusambaza kwa mofimu hii: lugha ya Kiswahili. Tena tunajua kwamba Kiswahili kilikuwa na kiambishi hicho tangu zamani sana. Tunataja majina ya miji miwili tu: mji wa “Quelimani”, yaani *kilimani*, huko Msumbiji; tena mji mkuu wa Visiwa vya Komoro, “Moroni”, yaani *motoni*. (Angalia kwamba shina la jina la mji na wa jina la visiwa ni ule ule *moro* au *moto*; *ku-moro* ni ngeli ya 17 ya Kibantu cha kawaida, *moro-ni* ni namna ya Kiswahili ya kutaja mahali. Kuna mlima mrefu wa volkeno huko katika kisiwa cha Ngazija.)

Kusema kwamba Kiswahili kimekuwa chombo cha kueneza kiambishi tamati cha mahali *-ini* si kusema kwamba Kiswahili kilikuwa lugha ya kutunga mofimu hiyo. Tungeweza kubuni mfululizo wa matukio ufuatao: Kiambishi *-ini* kilitokea kwanza katika lugha fulani, baadaye Kiswahili kilikopa mofimu hiyo, baadaye lugha nyingine ziliikopa kutoka kwa Kiswahili. Tunapotaka kuona lugha zipi zingeweza kuwa asili ya kiambishi tamati *-ini* inatubidi kutafuta lugha ambazo zina kiambishi hicho pamoja na neno *ini*.

Sasa, tukilinganisha orodha ya lugha yenye kiambishi tamati *-ini* (taz. Ramani 1) na lugha zenye neno *ini* (taz. Ramani 2) tunatambua kwamba zipo lugha chache tu ambazo zingeweze kuwa asili ya kiambishi tamati *-ini*. Hizo ni:

- lugha za Sabaki
- Kikikuyu
- Kisambaa

Tunachagua lugha za Sabaki — au pengine lugha ya Sabaki ya asili — kwa sababu mbili. Ya kwanza, inaelekea kwamba neno *ini* si ya zamani sana katika lugha za Kikikuyu na Kisambaa. Kikikuyu ni lugha ya pekee katika tawi la lugha za Kenya ya Kati yenye neno *ini*, na lugha ya Kisambaa pia ni lugha ya pekee katika tawi lake la “Seuta” ambayo ina neno *ini*.

Sababu ya pili inatokana na umbo. Kwa Kikikuyu, irabu ya mwisho ya neno *ini* si sawa na irabu ya mwisho ya kiambishi tamati *-ini*. Angalia kwamba lugha ya pekee katika kundi la Sabaki ambayo imehifadhi irabu saba ya Kibantu cha asili

ni Kiilwana; katika lugha hiyo kiambishi tamati cha mahali lina irabu *i* mwishoni, kwa mfano *nyuubeeni* 'nyumbani' (D. Nurse, mawasiliano ya binafsi). Tena, lugha za kundi la Kisotho/Kitswana (S.30) zimehifadhi irabu saba vilevile, na iko wazi kwamba kiambishi tamati chao cha mahali *-ŋ* kinatokana na **-ini* yenye irabu *i* mwishoni.

Kwa hiyo tunafikiri kwamba asili hasa ya kiambishi cha mahali ni Kiswahili. Pendekezo hilo lina matatizo matatu.

Shida ya kwanza ni ukubwa wa eneo la kiambishi hicho *-ini*. Shida hii inahusu hasa lugha za Afrika Kusini. Tunajua kwamba Waswahili wa zamani wamefika mpaka Msumbiji wa kati, yaani mpaka mdomo wa mto wa Zambezi, lakini hatuna ushahidi kwamba wamesafiri na kufanya biashara kusini zaidi. Hata hivyo, kuna maneno kama *imali* 'fedha' katika lugha ya Kizulu ambayo inaonyesha kwamba mawasiliano yalikuwepo.

Shida ya pili inahusu maana. Tumeona kwamba maana ya kiambishi tamati *-ini* inafanana na maana ya ngeli ya 18 *mu-*. Dhanio la Sacleux inaeleza vizuri ulingano huo: Maana ya neno *ini* inataja 'kiini' cha kitu. Kwa bahati mbaya, ulingano huo hauonekani wazi katika lugha ya Kiswahili ya siku hizi, lakini upo katika lugha ya Kitonga ambayo ni mbali sana ya Uswahilini. Inatubidi tuseme kwamba kiambishi tamati kilikuwa na maana ya undani chanzoni wakati wa kutawanyika, lakini baadaye maana hii ilipanuka katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Sabaki mpaka ikawa na maana ya mahali popote au kokote. Mifano tuliyoitaja juu kama *miongoni mwa* na *chini mwa* (kutokana na Kiswahili cha zamani) yangeweza kuimarisha dhanio hilo.

Shida la tatu linahusu umbo la kiambishi. Shida hilo linafanana na swali kuhusu maana: Umbo la kiambishi lilikuwa *-ini* kwa asili, lakini katika lugha ya Kiswahili ni *-ni* bila irabu mwanzoni. Tukifuata Sacleux tumeshafahamu asili ya ile irabu *i*: ilikuwa ni kiambishi awali cha ngeli ya 5. Wakati lugha nyingine zilipokopa mofimu hiyo umbo lake lazima lilikuwa bado *-ini*. Basi, kufuata kanuni za fonolojia ya Kiswahili tungetarajia kwamba tungesikia ***nyumbeni* badala ya *nyumbani*; linganisha irabu *e* katika hali ya kuamuru kwa wingi *piteni*. Lakini kama irabu ya mwisho wa kitenzi si *a* hatusikii dalili ya *i*, kwa mfano *jaribuni*. Kwa hiyo tunapendekeza kwamba umbo la kiambishi tamati cha mahali limesawazishwa likawa *-ni* baada ya jina lolote yenye irabu yoyote mwishoni.

Basi, ingawa hatuna hakika kamili juu ya asili ya kiambishi tamati cha mahali -ini inatuelekea kwamba kuna hoja za kutosha kuunga mkono na dhanio la Sacleux kuliko dhanio la Raum-Meinhof.

* Tunamshukuru Bi G. Scheckenbach (Bayreuth) ambaye anatumkumbusha kwamba katika lugha ya Kikinga (G.65), neno *untima* '(ma)ini' likitumika kwa njia ya sitiari lina maana ya mahali panapokaa hisia za binadamu kama hofu na woga.

Marejeo

- Dammann, Ernst. 1940. *Dichtungen in der Lamu-Mundart des Suaheli*. (Abhandlungen aus dem Gebiet der Auslandskunde der Hansischen Universität, 51.) Hamburg: Friederichsen, de Gruyter & Co.
- Grégoire, Claire. 1975. *Les locatifs en bantou*. (Annales, 83.) Tervuren: Musée royal de l'Afrique Centrale.
- Heine, Bernd, Ulrike Claudi na Friederike Hünemeyer. 1991. *Grammaticalization: a conceptual framework*. Chicago: The University of Chicago Press.
- Heine, Bernd, Tom Güldemann, Christa Kilian-Hatz, Donald A. Lessau, Heinz Roberg, Mathias Schladt and Thomas Stolz. 1993. *Conceptual shift: a lexicon of grammaticalization processes in African languages*. (Afrikanistische Arbeitspapiere, 34/35.) Cologne: Institut für Afrikanistik, Universität zu Köln.
- Krapf, Ludwig. 1882. *A dictionary of the Suahili language*. London. (Reprint Gregg Press 1964, Ridgewood, New Jersey.)
- Meinhof, Carl. 1941/42. Entstehung und Gebrauch der Lokativendung in Bantusprachen. *Zeitschrift für Eingeborenen-Sprachen* 32:161-164.
- Miehe, Gudrun. 1979. *Die Sprache der älteren Swahili-Dichtung (Phonologie und Morphologie)*. (Marburger Studien zur Afrika- und Asienkunde, A18.) Berlin: Dietrich Reimer.

- Ndalu, Ahmed, na Kitula G. King'ei. 1988; 1991. *Kamusi ya semi za Kiswahili*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Nurse, Derek, na Thomas J. Hinnebusch. 1993. *Swahili and Sabaki: a linguistic history*. Berkeley and Los Angeles: University of California Press.
- Raum, J. 1909. *Versuch einer Grammatik der Dschaggasprache (Moschi-Dialekt)*. (Archiv für das Studium deutscher Kolonialsprachen, 11.) Berlin: Georg Reimer.
- Sacleux, Ch. 1939. *Dictionnaire swahili-français*. Paris: Institut d'Ethnologie.
- Scheven, Albert. 1981. *Swahili proverbs: Nia zikiwa moja, kilicho mbali huja*. Washington, D.C.: University Press of America.